

## Maswali

1. Ibrahimu alimtakia Isaka mke wa aina gain?
2. Alimtuma nani kumtafutia Isaka mke?
3. Eliezeri alienda wapi?
4. Eliezeri aliomba nini?
5. Nani alitokea kwa kisima?
6. Rebeka alifanya nini?
7. Rebeka alikuwa binti wa nani?
8. Kaka wa Rebeka alikuwa nani?
9. Eliezeri alimpeleka Rebeka wapi?
10. Isaka alimpenda Rebeka?

## Majibu

1. Mwanamke aliyempenda Mungu.
2. Ibrahimu alimtuma Eliezeri kumtafutia Isaka mke
3. Eliezeri alienda Harani.
4. Kwamba Mungu amuonyeshe yule mke.
5. Rebeka alitokea kisimani
6. Rebeka aliwachotea Eliezeri na ngamia maji
7. Rebeka alikuwa binti wa Bethueli
8. Labani alikuwa kaka yake Rebeka.
9. Eliezeri alimpeleka Rebeka nyumbani kwao Isaka
10. Ndiyo Isaka alimpenda Rebeka.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM



**Awamu ya 1 Mwaka wa 1**

## 8 Isaka na Rebeka

### Marejeo

Mwanzo 24

### Kiini cha somo

Kuonyesha umuhimu wa kuoa mtu aliye na imani moja na wewe.

### Maneno maalum

1. Mke kwa Isaka+Mwanamke ampendaye Mungu + Eliezeri + Harani
2. Kisima cha maji + Maombi ya Eliezeri + Rebeka + Ngamia Wanakunywa + Bethuel
3. Pete ya pua + Makaribisho ya Labani
4. Safari Nyumbani + Harusi

**8.1** Ibrahimu alitaka mwanawe Isaka kuo mwanamke aliye na imani kwa Mungu. Hakutaka Isaka aoe mwanamke kutoka mataifa maovu waliokuwa wakikaa nao.

Ibrahimu alimtuma mtumishi wake Eliezeri kwa watu wake ili amtafutie Isaka mke.

“Mungu atatuma malaika wake kumchagulia Isaka mke,” Ibrahimu alisema.

Eliezeri alichukua ngamia kumi waliokuwa wamebeba zawadi na akaenda walikokaa jamaa wa Ibrahimu.

**8.2** Alipofika nje ya mji, alifanya ngamia wapige magoti karibu na kisima cha maji. Ilikuwa jioni wakati wanawake wanaenda kuteka maji.



Aliomba “Ee Bwana Mungu, nionyeshe mwanamwali (mke kijani) uliyemchagulia Isaka. Na awe ni yule mwanamke atakaye nipa maji ninywe na kuwapa ngamia pia.”

Eliezeri alikuwa bado anaomba, wakati Rebeka alitoka mjini na mtungi begani, alikuwa na sura nzuri.

“Tafadhali nisaide maji ninywe,” aliomba. “Kunywa,” Rebeka alisema, “nitawapa ngamia wako maji pia.”

Ngamia walipomaliza kunywa, Eliezeri alitoa pete ya dhahabu ya pua akampa Rebeka. “Wewe ni binti wa nani?” alimuuliza. “Mimi ni binti wa Bethuel, akasema “na huyu Betheul ni mtoto wa nduguye Ibrahimu.”

Eliezeri akainamisha kichwa na kusujudia Mungu kwa maana alikuwa amejibu maombi yake.

**8.3** Walienda kwa kina Rebeka, naye akaeleza mama yake na kaka yake Labani kila kitu. Mara tu, Labani alipoona pete ya dhahabu ya pua na zawadi zilizoletwa, alimkimbilia Eliezeri.

“Karibu ndani,” alisema, “tuna chumba chako na mahali pa ngamia.”

Walishusha mizizo kutoka kwa ngamia na kumtengenezea Eliezeri chakula. Eliezeri hakula mpaka aseme sababu iliyomleta.

**8.4** “Mimi ni mtumishi wa Ibrahimu,” alisema, “amenituma nije nimtafutie mwanawe mke. Na, ni lazima awe anayempenda Mungu.”

Labani na jamaa yake walifurahi “Mungu amefanya haya,” alisema, “Rebeka ndiye huyu, mchukue na uende, atakuwa mke wa mwana wa Ibrahimu.” Walisafiri kwa ngamia wakaenda anapoishi Ibrahimu. Isaka alipomuona Rebeka, alimpenda akawa mke wake.

